BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 21 Mei, 2025**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2025/2026.

III. **MASWALI:**

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

7. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

   Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa fursa sawa za ajira kwa watu wote wenye sifa wakiwemo watu wenye ulemavu.

   (a) Kwa namna gani Serikali imeimarisha mazingira ya kupatikana ajira kwa watu wenye ulemavu.

(b) Kwa namna gani mazingira ya kufanyakazi kwa watumishi wenye ulemavu yameimarishwa ndani ya utumishi wa umma.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

139. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wapo baadhi ya omba omba katika Manispaa ya Mjini hawana tatizo la ulemavu lakini hutumia mbinu hiyo kwa ajili ya kujipatia kipato.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya jambo hili ambalo linaanza kuchukua sura mpya.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

61 MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Lengo la Serikali yetu ni kukusanya mapato katika maeneo mbali mbali ya nchi hii zikiwemo bandari zetu na maeneo mengine.

Kuna mpango gani uliowekwa wa kukusanya mapato katika bandari zilizorasimishwa baada ya kumalizika ujenzi wake.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

177. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Ni yepi matarajio ya mradi mkubwa wa Mwinyi Housing Scheme katika kutatua changamoto ya makaazi bora kwa wananchi.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

275. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini ya tatizo la maradhi ya uti wa mgongo iko vipi kwa sasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

180. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni mambo gani ya kujivunia ya mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu yanayotokana na mchango mkubwa wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

131. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Shirika lake la Bandari, kwa kufanikiwa kutumika bandari ya Mkoani katika kupokea meli za makontena na kukabidhi bandari hiyo kwa muwekezaji husika.

(a) Je, mafanikio gani yaliyopatikana hadi sasa.

(b) Je, ni meli ngapi za makontena zimeingia nchini kupitia bandari ya Mkoani tangu alipokabidhiwa muwekezaji huyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

121. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tatizo la kuzagaa kwa wanyama hususani jamii ya mbwa nyakati za usiku linatishia na wakati mwengine huwajeruhi wananchi katika maeneo mbali mbali ya jimbo la Mwanakwerekwe.

Ni ipi kauli thabiti na ya kimkakati ya Serikali ya kupambana na kadhia hii iliyodumu kipindi kirefu hivi sasa.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

186. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ni matokeo gani chanya yamepatikana katika maendeleo ya jinsia, watoto na wazee mpaka muda huu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

145. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni watu gani mashuhuri wa kukumbukwa zaidi katika historia ya kumbukumbu ya Zanzibar kabla ya ujio wa wakoloni.

(b) Kwa kiasi gani historia ya urithi wa watu hawa inaenziwa ipasavyo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

294. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Moja ya changamoto inayochangia Zanzibar kutonufaika kikamilifu na rasilimali za uchumi wa buluu ni pamoja na kukosekana kwa mfumo jumuishi wa kitaasisi wa uratibu wa shughuli za uchumi wa buluu.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwa na mfumo jumuishi wa kitaasisi ili nchi inufaike zaidi na uchumi wa buluu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**21 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**